



Iowa City Community School District

Kituo cha Huduma za Elimu

Matt Degner Msimamizi wa Shule

1725 North Dodge Street • Iowa City, IA 52245 • (319) 688-1000 • Faksi (319) 688-1009 • www.iowacityschools.org

Usajili wa Chekechea

- Kwa:** Wazazi wa watoto watakaokuwa na umri wa miaka 5 mwezi wa Septemba au kabla ya tarehe **15 Septemba, 2022**
(Tarehe ya kuzaliwa ni au kabla ya 15/09/2017)
- Mint:** Msajili mtoto wako katika chekechea, kwenye shule ambayo ameruhusiwa kuhudhuria

Iowa City Community School District inatazamia kusajiliwa kwa mtoto wako wa chekechea mwakani. Yapo hapa baadhi ya maelezo ya jumla na tarehe muhimu.

Maelezo ya Jumla kuhusu Chekechea

Chekechea ni mpango wa siku nzima kwa watoto, siku tano kwa wiki. Iwapo kama mzazi, unapendelea mpango wa siku nusu kwa mtoto wako, hilo ni chaguo. Mfahamishe mwalimu mkuu wa shule yako kuhusu uamuzi wako. Iwapo mwanafunzi atahudhuria shule asubuhi, wazazi wamchukue mtoto wao kabla ya kishuka; iwapo mwanafunzi atahudhuria shule alasiri, wazazi wamlete mtoto wao baada ya kishuka. Lazima wazazi wachague iwapo ni kipindi cha asubuhi au ni cha alasiri na huenda wasibadilishe mahudhurio kati ya haya mawili. Usafiri ni jukumu la wazazi wakati mtoto anahudhuria siku nusu ya shule. Wazazi wanaochagua chekechea ya siku nusu lazima wajaze fomu ya wilaya ya Half- Day Preference na wanaweza kubadilisha pendeleo hili mara moja wakati wa mwaka wa shule hadi siku nzima.

Umri wa Kuingia

Miongozo ya Usajili wa Chekechea (Iowa Code 282.3)

- **Lazima wanafunzi wawe na miaka 5 kufikia tarehe 15 Septemba ili kujisajili katika chekechea.**
- Iwapo mwanafunzi **amekamilisha** chekechea katika shule ya umma au binafsi iliyo na kibali, katika jimbo au nje ya jimbo, **huenda** akasajiliwa katika daraja la kwanza hata iwapo hatakuwa na miaka 6 kufikia tarehe 15 Septemba.
- Iwapo mwanafunzi **hajakamilisha** chekechea (mfano, alitoka katikati ya mwaka) na hakuwa na miaka 5 kufikia tarehe 5 Septemba hawezi **kusajiliwa** katika chekechea kwenye Jimbo la Iowa. Hali hii hutokea wakati jimbo/nchi nyingine au shule ya binafsi iliyo na kibali, ina tarehe tofauti ya umri uliowekwa kwa usajili wa chekechea (kama vile miaka 5 kufikia tarehe 1 Novemba.)

Kuna Maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Iowa yanayoeleza kwamba hakuna aliye na uhuru wa kutozingatia sheria hii. Hakuna vighairi vinavyoruhusiwa ikiwa ni pamoja na watoto wanaokuja kutoka katika jimbo jingine ambalo mtoto amesajiliwa katika chekechea mara nyingi kwa mwaka.

- Kwa mujibu wa sheria ya shirikisho, watoto wa familia za majeshi lazima wasajiliwe katika daraja la kabla ya shule bila kujali umri.

Siku ya Kwanza ya Shule

Shule inaanza Jumanne, tarehe 23 Agosti, 2022.